



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UCHUKUZI  
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



**TAARIFA KWA UMMA**

**NJIA MPYA ZA USAJILI WA LESENI MKOANI DAR ES SALAAM**

*Dar es Salaam, 29 Novemba, 2024.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawakaribisha wasafirishaji kuomba leseni kwenye njia mpya za Daladala Jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kufikisha huduma karibu na wananchi kwa mabasi yanayokidhi vigezo kama ifuatavyo;

NA	KUTOKA	KWENDA	KUPITIA BARABARA YA	UJAZO WA BASI KUANZI A ABIRIA	IDADI
1.	MWENGE STENDI	BUNJU SOKONI	BAGAMOYO	25	20
2.	MWENGE STENDI	MBWENI MWISHO	BAGAMOYO	25	20
<b>KUONGEZA IDADI YA MAGARI</b>					
1.	MBEZI LUIS	MAKUMBUSHO	MOROGORO, KAWAWA, MWANANYAMALA	25	10

**Vigezo vya kuzingatia:**

- Magari yenye usajili kuanzia namba **EHA** kwa njia ya **Mbezi Luis – Makumbusho** kupitia barabara ya Morogoro, Kawawa, Mwananyamala.
- Magari yenye usajili kuanzia namba **DAA** kwa njia za **Mwenge Stendi – Bunju Sokoni** na **Mwenge Stendi – Mbweni Mwisho** kupitia barabara ya Bagamoyo.
- Kwa gari jipya ambalo halijawahi kusajiliwa katika mfumo wa utoaji leseni wa **RRIMS**, dereva wa gari husika atapaswa kuthibitishwa LATRA.
- Kwa magari ya njia ya Mbezi Luis - Makumbusho, leseni ni kwa muda wa mwaka mmoja na kuhuisha itategemea hali ya huduma za usafiri katika barabara tajwa.

**Imetolewa na:**  
**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**